



# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MAMLAKA  
YA MAWASILIANO TANZANIA (2022-2023) NA MAENDELEO  
YA SEKTA YA MAWASILIANO**

---

## 1.0 UTANGULIZI

Hii ni taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) katika kipindi cha mwaka wa fedha kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023 pamoja na maendeleo ya sekta ya mawasiliano kwa ujumla. TCRA ni Taasisi ya Serikali yenye jukumu la kusimamia Sekta ya Mawasiliano nchini Tanzania. Sekta ya Mawasiliano inajumuisha:

- (i) Sekta ndogo ya Simu na Intaneti
- (ii) Sekta ndogo ya Utangazaji
- (iii) Sekta ndogo ya Posta

TCRA ilianzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Namba 12 ya mwaka 2003 baada ya kuunganishwa kwa iliyokuwa Tume ya Utangazaji Tanzania (TBC) na Tume ya Mawasiliano Tanzania (TCC). TCRA ilianza kutekeleza majukumu yake tarehe 1 Novemba 2003.

### 1.1 Kazi na Majukumu ya TCRA

Kwa mujibu wa Kifungu Na. 5 cha Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na. 12 ya 2003, TCRA ina wajibu wa:-

- (i) Kuhimiza ushindani bora na uchumi wenye tija;
- (ii) Kulinda haki na maslahi ya watumiaji;
- (iii) Kuhamasisha upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa watumiaji wote ukijumuisha watumiaji wenye kipato kidogo, walioko vijijini na watumiaji ambao wako katika maeneo yasiyokuwa na mvuto wa kibiashara;
- (iv) Kuimarisha elimu kwa umma, uelewa na kuzifahamu huduma zinazosimamiwa na TCRA; na
- (v) Kuhakikisha umuhimu wa kulinda na kutunza mazingira.


Aidha, kwa mujibu wa Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania na *Sheria ya Mawasiliano Kielektroniki na Posta Na. 3 ya Mwaka 2010*, majukumu ya TCRA ni pamoja na:-

- (a) Kutoa leseni, kuongeza muda wa leseni na kufuta leseni pale ambapo masharti ya leseni husika hayafuatwi;
- (b) Kuweka viwango, kanuni na masharti ya kusambaza bidhaa na huduma zinazosimamiwa;
- (c) Kudhibiti viwango na bei ya jumla ya mawasiliano kati ya mitandao.
- (d) Kufuatilia utendaji na mwenendo wa Sekta ya Mawasiliano;
- (e) Kuwezesha kutatuliwa kwa malalamiko na migogoro baina ya Watoa huduma na kati ya Mtoa huduma na Mtumiaji wa huduma;
- (f) Kufanya mashauriano na taasisi nyingine za udhibiti, Bodi au Taasisi zenye majukumu yanayofanana na yale ya TCRA katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na nje ya nchi;

TCRA ina Ofisi Tanzania Bara na Visiwani kama inavyoonekana hapa chini:-

KANDA	MIKOA
OFISI YA ZANZIBAR	Unguja Kaskazini na Unguja Kusini, Pemba Kaskazini, Pemba Kusini, <b>Unguja Mjini Magharibi</b>
MASHARIKI	<b>Dar es Salaam</b> , Morogoro, Lindi, Pwani na Mtwara
KASKAZINI	<b>Arusha</b> , Manyara, Kilimanjaro, Tanga
ZIWA	<b>Mwanza</b> , Geita, Kagera, Shinyanga, Mara, Simiyu
KATI	<b>Dodoma</b> , Singida, Tabora, Kigoma
NYANDA ZA JUU KUSINI	Mbeya, Songwe, Iringa, Ruvuma, Rukwa, Katavi, Njombe

Shughuli za Mamlaka ya Mawasiliano zinagusa wadau wakuu watatu ambao ni **Serikali** yenye jukumu la kutoa sera na sheria; **watoa huduma** wanaopewa leseni na masharti ya namna ya kutoa huduma husika, na **watumiaji wa huduma za mawasiliano** ambao TCRA ina jukumu la kulinda maslahi yao kwa kuhakikisha upatikanaji wa huduma zenye ubora, usalama na kwa bei nafuu.



Taasisi ambazo ni wadau wa moja kwa moja na TCRA kiutendaji ni pamoja na Tume ya Utangazaji Zanzibar (ZBC), Vyombo vya kusimamia sheria, Tume ya Ushindani wa Biashara (FCC), Baraza la Ushindani (FCT), Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA-CCC), Benki Kuu ya Tanzania (BOT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Msaliji wa Hazina, n.k.

## 1.2 Dira, Dhamira na Lengo Kuu la Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)

**1.2.1 Dira:** Jamii iliyowezesha na huduma za mawasiliano.

**1.2.2 Dhamira:** Kusimamia huduma za mawasiliano kwa ustawi wa Jamii ya Watanzania.

**1.2.3 Lengo Kuu:** Kuimarika na kuendelezwa kwa utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote na kwa gharama nafuu.

### 1.3 Sekta ya Mawasiliano na Mchango wake Katika Uchumi

Sekta ya Mawasiliano ni Sekta wezeshi inayochangia kukua na kuendelea kwa sekta nyingine. Huduma na bidhaa za Mawasiliano ni za msingi katika maisha ya wananchi kisiasa, kijamii na kiuchumi.

Kutokana na mchango huo, Sekta ya Mawasiliano imekuwa ya kimkakati na ya msingi katika maendeleo ya uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu nchini Tanzania; kuanzia ngazi ya mtu binafsi, ngazi ya Kaya, Taasisi na Kitaifa.

Utoaji wa huduma za mawasiliano ni wa ushindani hivyo umesababisha kuongezeka kwa idadi ya mitandao, matumizi ya TEHAMA na aina za huduma zinazotolewa kwa Wananchi, Taasisi na Serikali kwa ujumla. **Kuenea kwa huduma hizi kunawezeshwa na uwepo wa Sera imara, sheria nzuri na mifumo wezeshi ya kiusimamizi na utoaji leseni.**

TCRA imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia malengo yaliyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III) kwenye sekta ya mawasiliano, ambayo utekelezaji wake unahusisha mchango wa TCRA kwenye uchumi kama ifuatavyo:-

- (a) Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano na upatikanaji wa huduma za mawasiliano kwa lengo la kuboresha uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu;
- (b) Kuendelea kuweka mazingira bora ya ushindani kwenye sekta ya mawasiliano ili wananchi wengi waweze kumudu gharama za huduma za mawasiliano;
- (c) Kulinda watumiaji wa huduma za mawasiliano dhidi ya uhalifu mtandaoni kwa kutumia mifumo ya kiusimamizi; na
- (d) Kugawa rasilimali za mawasiliano, ikiwa ni pamoja na masafa na kutoa leseni kwa watoa huduma zinazowezesha kuongeza idadi ya watumiaji wa intaneti ili kufikia lengo la asilimia 80 ifikapo 2025.

## 2.0 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA

### 2.1 Huduma kwa wateja

TCRA imethibitishwa na Shirika la Viwango la Kimataifa la ISO 9001:2015 kutokana na ufanisi katika kumhudumia mteja. Katika kuhakikisha wateja wanahudumiwa ipasavyo, TCRA imeendelea kuboresha mifumo ya huduma kwa wateja kama ifuatavyo:

(a) **“Tanzanite Portal”**: TCRA imeongeza ufanisi katika kuhudumia mteja kupitia dirisha moja la maombi ya leseni za aina zote, utoaji wa vyeti vya uhakiki wa vifaa vya kielektroniki, anuani za makazi na dawati la huduma kuwezesha mawasilisho ya malalamiko ya wateja. Kwa kupitia “Tanzanite portal” wateja wamehudumiwa katika maeneo yafuatayo:-

- (i) Maombi ya leseni na nambari za mawasiliano bila kufika kwenye ofisi za TCRA;
- (ii) Upangaji, ugawaji na ufuatiliaji postikodi za anwani za makazi ambapo watumiaji (wananchi) walipata postikodi za maeneo mbalimbali kupitia tovuti ya TCRA;
- (iii) Kushughulikiwa kwa maoni, changamoto na taarifa mbalimbali kutoka kwa wateja na wanaotaraji kupata huduma za TCRA;
- (iv) Kujitambulisha TCRA kwa kubainisha leseni walizonazo, taarifa za kampuni pamoja na taarifa za malipo;
- (v) Kushughulikiwa kwa maombi ya kufanya uhakiki wa vifaa vya kielektroniki (Online Type Approval).

#### (b) Dawati la Huduma kwa Mteja

- TCRA imeboresha Dawati la Huduma kwa Wateja ambalo linafanya kazi ya kuhakikisha msaada unatolewa kwa watoa huduma pale wanapokutana na changamoto katika utoaji wa huduma au kupata huduma mbalimbali za Mamlaka.
- TCRA imeendelea kuisitiza matumizi ya namba maalumu ya kupiga simu bure ambayo ni **0800008272** ili kuwahudumia wateja wake kwa karibu ikiwa ni pamoja na kutoa taarifa mbalimbali kwa wawekezaji juu ya kupata leseni, kupata taarifa

muhimu za watoa huduma na kushughulikia malalamiko mbalimbali ikiwa ni pamoja na kushughulikia rufaa zinazoletwa na watumiaji wa huduma za mawasiliano, ambayo hayakupatiwa ufumbuzi wa kuridhisha kwa watoa huduma wao.

- Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2022 hadi kufikia Juni, 2023, TCRA ilipokea na kuwahudumia jumla ya **wateja 5,695**.

## 2.2 Utoaji wa Leseni

TCRA imeendelea kutoa Leseni na kusimamia masharti ya leseni kwa watoa huduma za mawasiliano nchini. Hadi kufikia Juni 2023, tunawatoa huduma **1481 na jumla ya leseni 2,415**. TCRA imetoa leseni zifuatazo:

### Jedwali Na 1: Leseni zilizotolewa

Na.	AINA YA LESENI	LESENI 2022/23	JUMLA YA LESENI MPAKA SASA
1	Miundombinu ya Mawasiliano (Network Facilities License)	1	31
2	Utumiaji wa Miundombinu ya Mtandao (Network Services)	0	16
3	Matumizi ya Huduma (Application Services)	16	127
4	Huduma za Maudhui (Content Services)		
	✓ Televisheni	6	66
	✓ Televisheni za Mtandaoni (Online TV)	67	272
	✓ Cable TV	17	81
	✓ Redio	21	225
5	Posta na Ushafirishaji Vifurushi (Postal & Courier Services)		
	✓ Mtoa Huduma wa Umma (Shirika la Posta Tanzania)	0	1
	✓ Kampuni binafsi za usafirishaji (Couriers)	48	104
6	Leseni ndogo za Ufungaji na Utengenezaji, Uingizaji na Usambazaji wa Vifaa vya Simu, VSAT, Masafa ya VHF/HF/UHF, na Namba za Kieletroniki	571	1,484
<b>JUMLA</b>		<b>749</b>	<b>2,415</b>

### 2.3 Ufuatiliaji na Utekelezaji

Katika kipindi cha kuanzia Julai 2022 mpaka Juni 2023, TCRA imeendelea kuwasimamia watoa huduma za mawasiliano kwa kuhakikisha wanatoa huduma kwa mujibu wa masharti ya leseni zao pamoja na kuzingatia viwango vya ubora ambavyo vimewekwa kwenye kanuni na sheria zinazoongoza sekta ya mawasiliano nchini. Aidha tumefanya maboresho makubwa ya mifumo ya udhibiti wa Sekta ambapo kwa sasa tumejenga uwezo wa kufuatilia ubora wa huduma tukiwa ofisini, ili kuhakikisha watoa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti, utangazaji (Radio na Televisheni) na posta wanatoa huduma kwa ufanisi na kwa kuzingatia ubora. Aidha, TCRA ilifanya ufuatiliaji na kuhakikisha utekelezaji wa masharti ya kanuni na sheria katika maeneo yafuatayo:-

**(a) Ukaguzi wa watoa huduma:-** TCRA imefanya ukaguzi kwa watoa huduma **671** wa **simu na intaneti, utangazaji na posta** ili kuhakikisha wanatoa huduma kwa mujibu wa sheria, kanuni, miongozo na masharti ya leseni. TCRA ilitoa maelekezo, onyo, na adhabu kwa watoa huduma waliokutwa na ukiukwaji wa sheria, kanuni, miongozo na masharti ya leseni.

**(b) Upimaji wa Ubora wa huduma za mitandao ya simu:-** TCRA imefanya upimaji wa ubora wa huduma za mawasiliano ya simu katika **mikoa ishirini na nne (24), Tanzania Bara** na mikoa yote ya **Zanzibar**. Pia, TCRA imekuwa ikikutana na watoa huduma za mawasiliano ya simu na intaneti kila robo mwaka kujadili matokeo ya upimaji wa ubora wa mitandao ya simu na kukubaliana hatua za kuchukua kufanya maboresho ili kuongeza ubora wa huduma za simu za sauti (voice), data, na ujumbe mfupi (SMS).

Upimaji wa hivi karibuni ulifanyika kuanzia mwezi **Aprili** hadi **Juni, 2023** umehusisha **makampuni (06) ya simu** katika maeneo ya **miji saba (07)** ambayo ni **Kahama, Songwe, Mbeya, Kigoma, Katavi, Tabora, and Rukwa**. Taarifa za matokeo ya upimaji wa ubora wa huduma za mawasiliano na maendeleo ya sekta zinapatikana kupitia viunganisho vifuatavyo:-

1. <https://t.ly/nLrwl> (Taarifa ya Maendeleo ya Sekta Aprili-Juni 2023)
2. <https://t.ly/Hpob6> (Matokeo ya Upimaji wa Ubora wa Mawasiliano ya simu Aprili - Juni 2023)



**(c) Ukaguzi wa masafa :** TCRA hutekeleza ukaguzi wa masafa kwa kila robo mwaka kujua kiwango cha matumizi ya masafa iliyoyagawa kwa watoa huduma nchi nzima na kuhakikisha hakuna muingiliano wa masafa. TCRA imeendelea kutatua changamoto za muingiliano wa masafa zilizoletwa na watoa huduma na zilizoonekana wakati wa upimaji kama vile muingiliano wa masafa yanayotumika kwa huduma za mawasiliano ya ndege ili kuhakikisha usalama kwa huduma hiyo, muingiliano katika masafa ya radio ili kuhakikisha ubora wa usikivu na muingiliano wa masafa ya simu ili kuboresha huduma za simu.

**(d) Ufuatiliaji wa maudhui ya Redio na Televisheni:-** TCRA imekuwa inafanya ufuatiliaji wa maudhui ya redio na televisheni kuhakikisha watoa huduma wanarusha maudhui yanayoendana na sheria, kanuni na miongozo ya utangazaji. **Watoa huduma 152** walikutwa na makosa ya urushwaji wa maudhui yasiyofaa na hatua zimechukuliwa dhidi yao ikiwa ni pamoja na kupewa onyo, adhabu au maelekezo kwa mujibu wa sheria.

**(e) Upimaji wa Mionzi ya masafa ya redio na simu:-**

TCRA imefanya upimaji wa kiwango cha mionzi ya masafa ya redio na simu kwa **mikoa kumi na tano (15) Tanzania** ili kuwalinda watumiaji wa huduma za mawasiliano na wananchi wanaoishi karibu na miundombinu ya minara ya Simu, Redio na Televisheni. Upimaji wa kuhakiki kiwango cha mionzi itokanayo na minara/vifaa vya mawasiliano (Radio Frequency Electro Magnetic Field radiations - EMF). Vipimo hivi vilifanyika katika bandi mbalimbali zinazotumika kutoa huduma za mawasiliano ya Simu, Redio na Televisheni na matokeo yalikuwa ni kama ifuatavyo:-.

- Kiwango cha juu katika bandi ya FM Radio (87.5- 108 MHZ) kiwango kilikuwa **4.986 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni **27.7 V/m**.
- Katika bandi ya ya matangazo ya television (TV UHF (DTT) - 470 – 694 MHZ) kiwango kilikuwa **4.928 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya

kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni **29.8 V/m**.

- Katika bandi ya huduma za data LTE (Digital Dividend II - 694 – 790 MHZ) kiwango kilikuwa **3.823 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni **36.2 V/m**.
- Katika bandi ya huduma za data LTE (Digital Dividend I - 790 - 862 MHZ) kiwango kilikuwa **5.738 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni **38.6 V/m**.
- Katika bandi ya mawasiliano ya simu (GSM 900: 925 - 960 MHZ) kiwango kilikuwa **4.644 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni **41.8 V/m**.
- Katika bandi ya mawasiliano ya simu (GSM 1800: 1805- 1880 MHZ) kiwango kilikuwa **4.659 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP) ambacho ni **58.4 V/m**.
- Katika bandi ya mawasiliano ya simu na data (WCDMA/UMTS): 2110-2170 MHZ) kiwango kilikuwa **6.807 V/m (Volt per Meter)** ambacho ni chini ya kiwango cha juu kama ilivyoelekezwa na **International Commission on Non-Ionizing Radiation Protection (ICNIRP)** ambacho ni **63.2 V/m**.

Hali hii inaashiria kuwa, kiwango cha mionzi kutoka kwenye minara ya huduma mbalimbali za mawasiliano zilizopimwa **hakijavuka kiwango cha juu cha mionzi kama ilivyoelekezwa na ICNIP hivyo kuwa salama kwa watumiaji wa huduma za mawasiliano.**

**(f) Ufuatiliaji wa usambazaji wa miundombinu ya mawasiliano:** TCRA ikishirikiana na UCSAF zimekuwa zikifanya ukaguzi nchi nzima kuainisha maeneo yenye huduma hafifu na yasiyo na huduma za mawasiliano ya simu na intaneti. Maeneo haya huwasilishwa kwa watoa huduma kwa ajili ya taratibu za uboreshaji wa huduma kwenye maeneo hayo au kuwasilishwa UCSAF kwa ajili ya taratibu za ujenzi wa miundombinu mipya kwenye maeneo ambayo hayana mvuto kiuwekezaji kwa watoa huduma.

## 2.4 Upangaji na Usimamizi wa Rasilimali za Mawasiliano

Rasilimali za mawasiliano ni pamoja na **masafa, namba, viko, postikodi na anwani za makazi**. TCRA imeendelea kuhakikisha uwepo wa rasilimali zinazowezesha mawasiliano ya simu, Intaneti, redio na televisheni. Usimamizi wa rasilimali hizi umeweza kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

### (a) Masafa

Upangaji na usimamizi mzuri wa rasilimali za mawasiliano (masafa na namba), ndio unaowezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano pamoja na huduma za pesa mtandao. TCRA imefanikiwa kugawa masafa yanayowezesha utoaji wa huduma ya intaneti ya kasi. Jitihada hizi zitawezesha wananchi wengi kupata huduma za intaneti ya kasi ambayo ni muhimu sana wakati huu tukiwa kwenye uchumi wa kidijiti. Malengo ya Serikali ni kuhakikisha kuwa, ifikapo mwaka **2025** asilimia **80** ya Wananchi wanapata huduma ya intaneti ya kasi. Tunamshukuru Mhe. Rais kwa kuendelea kufungua fursa za milango ya TEHAMA ili kufikia lengo hili.

### (i) Rasilimali masafa kwa Intaneti ya Kasi

TCRA pamoja na kuweka mazingira mazuri ya kiusimamizi imetoa rasilimali masafa katika bendi za **700MHz, 2300MHz, 2600MHz na 3500MHz** yanayowezesha **intaneti ya kasi ya 4G na 5G**. Kuwepo kwa Intaneti ya kasi kunawezesha uchumi wa kidijiti katika maeneo mbalimbali kama vile Huduma za kifedha, utalii, kilimo na huduma za afya. ***Aidha, TCRA ipo katika hatua za awali za kufungua bendi za masafa ambazo zitatumiwa na watoa huduma bure bila kuhitaji kuwa na leseni ya rasilimali masafa (Unlicensed bands),***

***hatua hii itaongeza matumizi ya Intaneti kwa kuwa na huduma za intaneti za wazi (WiFi -hotspots).***

**(ii) Rasilimali Masafa ya Utangazaji wa Redio**

TCRA ilitangaza masafa ya utangazaji wa redio katika **mikoa 21 ya Tanzania** bara ambapo jumla ya **watoa huduma thelathini (30)** walipata nafasi ya kuanzisha vituo vya utangazaji wa redio katika maeneo mbalimbali. Uanzishwaji wa vituo vya utangazaji unachochea maendeleo katika jamii kwa kutoa elimu, kuhabarisha na kuburudisha.

**(b) Namba na Anuani za Mtandao**

TCRA hupanga na kutoa namba zinazotumika katika mawasiliano pamoja na namba fupi (short codes) zinazotumika katika kufanya miamala ya kifedha na kuwezesha huduma nyingine za ziada. TCRA imefanikiwa kufanya mambo yafuatayo kwenye rasilimali za namba:-

- (i) Kupanga na kugawa namba za huduma mbalimbali kwa watoa huduma kama vile huduma za ziada (VAS services), mawasiliano ya mashine (M2M services), namba za kupigwa bure (toll free numbers) nk.
- (ii) Imeandaaa Mkakati wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mabadiliko ya Anwani za Intaneti (IP addresses) **kutoka IPv4 kwenda IPv6**, ili kuongeza wigo wa watumiaji wa intaneti na kuwezesha mawasiliano ya vifaa kwa vifaa (internet of things);
- (iii) Kusimamia mitambo ya kuunganisha watoa huduma za Intaneti nchini (Internet Exchange Points – IXPs) ili kuhakikisha mawasiliano ya ndani ya nchi yanabakia nchini. **Trafiki ya mawasiliano ya Intaneti ya ndani ya nchi yameongezeka kutoka 19.4Gbps za mwaka jana na kufikia 32Gbps**, ongezeko hili linaashiria ongezeko la maudhui ya ndani ya nchi (local content) kwenye mtandao wa intaneti;
- (iv) Kukamilisha maandalizi ya mpango wa Taifa wa mawasiliano ya dharura (National Emergency Telecommunication Plan - NETP), ambao umeidhinishwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na upo tayari kwa utekelezaji;

- (v) Kusimamia utekelezaji wa nambari za maisha na usalama (Life and safety numbers), hususani kuwezesha kufikisha **miito ya huduma za dharura (190)** kwenda kwenye kituo maalumu cha ofisi ya Waziri Mkuu kinachohusika na majanga.

### (c) Vikoa vya dot TZ

TCRA katika kusimamia vikoa vya dot TZ imefanikisha mambo yafuatayo: -

- (i) Kuongeza usajili wa vikoa na **kufikia 28,076** ukilinganisha na **vikoa 24,749** vilivyosajiliwa kipindi cha mwaka 2021/22. Hili ni ongezeko la vikoa **3,327** sawa na **11.8%**;
- (ii) Kuimarisha **usalama wa vikoa 1,025** vilivyowekewa viendelezi vya usalama vya mfumo wa majina ya vikoa (DNSSEC), hii ikijumuisha vikoa takribani vyote vya serikali (go.tz);
- (iii) Kuidhinisha vyeti vya ithibati kwa **wasajili wapya sita (6)** wa vikoa vya dot TZ kufikisha idadi ya **wasajili sitini na tisa (69)**.

### (d) Postikodi

Postikodi ni rasilimali muhimu ya mawasiliano katika anuani za makazi. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania imefanikisha mambo yafuatayo: -

- (i) Kuhuisha kiwango cha anwani za makazi cha mwaka 2015 (Rural and Urban Addressing Standard **TZS1571:2015**);
- (ii) Kuhuisha na kuchapisha orodha ya postikodi;
- (iii) Imwezesha wananchi kutambua postikodi zao kwa kutumia mfumo mahsusi wa USSD. **Jumla ya sms 203,221 ziliweza kujibiwa kwa wananchi.**

Aidha, **TCRA inatoa rasilimali hizi bure** kwa wabunifu (Start-ups) mbalimbali wanaohitaji kufanya majaribio (testing) kwenye huduma zao kwa kipindi maalumu. Hadi kufikia Juni, 2023 TCRA imetoa rasilimali namba kwa ajili ya majaribio ya bunifu kwa wabunifu (start-

ups) wapatao wanne (4). **TCRA inatoa wito kwa vijana wajasiriamali, wabunifu na watafiti kuwasilisha wazo COSTECH na wakishapitishwa wanapatiwa rasilimali hizi bure.**

**(e) Uidhinishaji na usanifu wa vifaa vya Mawasiliano**

Vifaa vyote vya mawasiliano vinavyoingia nchini, lazima viidhinishwe na mamlaka kabla havijaanza kutumika ili kujiridhisha usalama wa vifaa hivyo kwa watumiaji na pia kuhakikisha havitasababisha muingiliano wa mawasiliano upande wa masafa (interference). TCRA ilipokea maombi **544** ya kuingiza vifaa vya Mawasiliano nchini. Maombi **50** yalipokelewa kipindi cha mwaka 2021/22 na kumalizika mwaka 2022/23. Jumla ya maombi yaliyofanyiwa kazi yalikuwa ni **594**. Kati ya maombi hayo, **vifaa vilivyoidhinishwa vilikuwa ni 511, na vifaa vilivyokataliwa kwa sababu mbalimbali vilikua 15.** Maombi **68** bado yanafanyiwa kazi. Aidha, TCRA inaendelea kufanya maboresho ya maabara na vifaa ili kuendana na mabadiliko ya teknolojia.

**(f) Usimamizi wa taka za vifaa vya Mawasiliano**

TCRA imeanza ukaguzi wa awali na utoaji wa cheti kwa vifaa vya mawasiliano vinavyoingia nchini ili kujiridhisha kwamba havijafikia mwisho wa matumizi yake, na pia kupitia utaratibu wa jinsi ya kuviteketeza pale vinapofikia ukomo wa matumizi, bila kusababisha madhara kwa watumiaji kwa mujibu wa sheria.

Ukaguzi huu unaenda sambamba na ukusanyaji wa awali wa gharama kwa ajili ya kugharamia utaratibu huu wa kuharibu vifaa vilivyoisha muda wake. Gharama hii hutozwa kwa watengenezaji wa vifaa vya kieletroniki ambao wengi wako nje ya nchi. Zoezi la ukaguzi wa awali na ukusanyaji wa gharama hizi linafanywa na kampuni ya **Bureau Veritas Tanzania Limited** kwa niaba ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na limeanza rasmi tarehe **23 Mei 2023.**

**2.5 Usimamizi wa shughuli za Mawasiliano ya Simu na Intaneti**

TCRA inatumia mfumo wa kusimamia na kuratibu mawasiliano yote na kubaini takwimu mbalimbali zinazopita katika mitandao ya mawasiliano. Mfumo huu unachukua taarifa kutoka kwenye mifumo ya watoa huduma, unazichakata na kutoa taarifa zinazoweza TCRA kusimamia majukumu yake ya kiudhibiti pamoja na


uhakiki wa taarifa za mapato ya watoa huduma za mawasiliano. Aidha, kupitia Mfumo huu umewezesha yafuatayo:-

**(a) Usimamizi wa simu za ndani na kimataifa:**

- (i) Idadi ya dakika za simu za kimataifa zinazolingia nchini (International Incoming) zimepungua kutoka **dakika 3,136,692 mwezi Julai 2022 hadi kufikia 2,900,165 mwezi Juni 2023 ambayo ni sawa na asilimia 7.54%**, idadi ya dakika za simu za kimataifa zinazotoka nchini (International Outgoing) zimepungua kutoka dakika **2,405,522 mwezi Julai 2022 hadi kufikia dakika 2,226,071 mwezi Juni 2023 ambayo ni sawa na asilimia 7.46%**. Kupungua kwa simu za kimataifa kunasababishwa na mabadiliko ya teknolojia na upatikanaji wa chaguzi mbadala za kupiga simu kupitia mitandao ya intaneti kama vile *Whatsap, Facebook, Telegram, Zoom* nakadhalika.
- (ii) Idadi ya dakika za simu za kitaifa ndani ya mtandao mmoja (onnet) zimeongezeka **kutoka dakika 6,172,696,579 mwezi Julai 2022 hadi dakika 7,012,574,045 mwezi Juni 2023 ambayo ni sawa na 13.61%**.
- (iii) Hivyo hivyo idadi ya dakika za simu za kitaifa nje ya mtandao mmoja (offnet) zimeongezeka kutoka **dakika 4,879,102,325 mwezi Julai 2022 hadi kufikia dakika 5,064,800,480 kufikia mwezi Juni 2023 ambayo ni sawa na 3.81%**. Ongezeko la simu za kitaifa linasababishwa na ukuaji wa sekta ya mawasiliano nchini.

**(b) Kubaini simu za ulaghai**

TCRA imeendelea kubaini simu za ulaghai zinazolingia hapa nchini na hatua stahiki zimekuwa zikichukuliwa. Kutokana na hatua hiyo, idadi ya simu za udanganyifu imeendelea kupungua kuanzia mwaka 2020 hadi Juni 2023. Hata hivyo, tulibaini matukio machache ya simu za ulaghai yalitokea mwezi Septemba, 2022 kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.



**(c) Kubaini na kufungia Vifaa vya Mawasiliano vyenye matatizo au visivyokidhi Ubona:** TCRA imesimamia zoezi la kuzuia matumizi ya simu zilizoripotiwa kuibiwa, kupotea au kuharibika pamoja na kuzuia matumizi ya simu zisizokuwa na viwango. Usimamizi huu unawezesha kubaini na kufungia namba tambulishi za vifaa vya Mawasiliano zilizopakiliwa (Duplicate International Mobile Equipment Identity-IMEIs), namba tambulishi za vifaa vilivyotumika kwenye udanganyifu pamoja na namba tambulishi zilizotolewa taarifa ya kupotea au kuibiwa.

Kuanzia Julai 2022 hadi kufikia Juni 2023 jumla ya **namba tambulishi zilizofungwa na mfumo huu ni 108,395** ambazo ziliripotiwa kupotea, kuibiwa au kuhusika katika matukio ya kihalifu, hivyo kuwezesha kupunguza matukio ya wizi na kusaidia upatikanaji wa vifaa vya Mawasiliano vyenye ubora kwenye soko.

**(d) Usimamizi wa Taarifa za Huduma za Miamala ya Fedha**

TCRA imesimamia taarifa za huduma za miamala ya fedha kupitia mitandao ya simu na kuwezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za miamala hivyo. Usimamizi huu umefanikisha yafuatayo:-

- (i) Idadi ya miamala kwa kipindi kilichoishia Juni 2022 ilikuwa **3,767,732,264** na mpaka kufikia Juni 2023 ilikuwa **4,670,491,000** sawa na ongezeko la 24%. Aidha, akaunti za pesa kwa simu pia zimeongezeka kwa **24%** kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023;



(ii) Vivyo, hivyo tozo ya miamala ya fedha kupitia simu za mkononi **imepungua** kutoka **19,225,082,685** mwezi Julai 2022 hadi kufikia **14,805,512,341** mwezi Juni 2023 ambayo ni sawa na **22.99%**. Kupungua kwa tozo ya miamala ya fedha imesababishwa na kupungua kwa viwango vya tozo ya miamala ya fedha vilivyoanza kutumika tarehe 1 Oktoba 2022.

#### (e) Usajili wa Laini za Simu

TCRA kwa kushirikiana na Mamlaka ya Vitambulisho Vya Taifa (NIDA), watoa huduma na wadau wengine ina jukumu la kusimamia usajili wa laini za simu. Aidha, laini zipatazo **milioni 7.3** zimesajiliwa kati ya mwezi Julai 2022 mwezi Juni 2023 ambayo ni sawa na **ongezeko la idadi ya laini za simu kutoka Milioni 56.7 mwezi Julai 2022 hadi kufikia idadi Milioni 64.1** mwezi Juni 2023 **sawa na ukuaji wa 13%**.

#### (f) Ufuatiliaji wa taarifa za miundombinu ya watoa huduma

TCRA imeendelea kusimamia na kufuatilia miundombinu ya mawasiliano ikiwa ni pamoja na usambaaji wa minara, miundombinu ya mkongo (fiber optic) pamoja na vituo vya kuhifadhi taarifa (Data centers) hivyo kupelekea kutambua ufikiwaji wa huduma katika maeneo mbalimbali nchini.

Aidha, tunashukuru Serikali ya awamu ya sita kwa kuona umuhimu wa kupunguza gharama za kupata kibali cha kupitisha miundombinu kwenye barabara (Right of Way Charges), ambapo hapo awali watoa huduma walitakiwa kulipa ada ya **malipo ya kujenga ya Dola za Kimarekani 1000 kwa Kilomita 1 na kila mwaka kulipia Dola za Kimarekani 1000 kwa Kilomita 1**. Gharama hizi zilikuwa zinachangia gharama za uendeshaji kuwa kubwa.

Kuazia julai,2023 Gharama zimepungua ambapo kwa kulipa ada ya malipo ya kujenga imekuwa **Dola za Kimarekani 200 na malipo ya kila mwaka ni Dola za Kimarekani 100**.

***Ni matarajio yetu kuwa, kupungua kwa gharama hizi kutapunguza gharama za uendeshaji na hivyo kuchochea kupungua kwa gharama za huduma za mawasiliano.***

## **2.6 Usimamizi wa Huduma za Utangazaji**

Utangazaji ni njia pekee ya Mawasiliano inayowafikia watu wengi kwa haraka na wakati mmoja. TCRA ina wajibu wa kuweka mazingira rafiki ya kusambaza huduma za Utangazaji kwa njia ya redio, televisheni na mitandao nchi nzima ili kumfikia kila mwananchi.

Hali kadhalika TCRA ina wajibu wa kuhakikisha kuwa maudhui yanayorushwa na vituo vya Utangazaji yanazingatia maadili na weledi wa uandishi wa habari na pia hayakiuki Sheria na Kanuni zinazosimamia Sekta ya Utangazaji. Pia ni wajibu wa TCRA kuhimiza utengenezaji, uzalishaji na usambazaji wa maudhui ya ndani (local content) na kutangaza urithi, vivutio, **mila na desturi za Mtanzania**. Kwa kipindi cha mwaka huu mambo yafuatayo yamefanyika :-

### **(a) Kuanzishwa kwa Vipindi vya Maadili**

Katika jitihada ya kujenga jamii ya Ki-Tanzania yenye maadili mema, **vituo 14 vyenye leseni ya Kitaifa** vinarusha vipindi vinavyotoa elimu ya malezi bora ya familia na vijana. Vilevile, TCRA kwa kushirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, na Makundi Maalumu inaratibu programu maalumu ya kuandaa vipindi vya maadili vitakavyorushwa na vituo vya Utangazaji **150 vyenye leseni ya Kiwilaya**. Mpango huu umelenga kushirikisha na kutumia vyombo vya Utangazaji vilivyopo kwenye maeneo ya Wilaya zetu kutoa elimu na kujenga jamii inayozingatia maadili, mila desturi na utamaduni wa mtanzania.

### **(b) Vipindi vya Katuni za Watoto na Ngoma za Asili**

Katika jitihada za kupambana na maudhui yanayotoka nje ya nchi ikiwa ni pamoja na Katuni za watoto zisizo na maadili ya Kitanzania, TCRA kwa kushirikiana na Wazalishaji Maudhui binafsi (Independent Producers) imeratibu uzalishaji wa vipindi vya Katuni za watoto zenye ubora wa hali ya juu ili watoto waweze kulishwa maudhui ya ndani. Pia TCRA inaratibu zoezi la kurekodi ngoma za **asili za makabila 120** kwa ubora wa hali ya juu ili

kukuza utamaduni wa nchi yetu. TCRA imeshirikiana na TBC na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM).

***Tunatoa rai kwa Vyombo vya utangazaji kuendelea kuzingatia sheria, kanuni na weledi katika kutoa maudhui, vilevile kwa wananchi kutosambaza maudhui ambayo ni yanakiuka misingi ya sheria, mila na desturi za Taifa la Tanzania.***

## **2.7 Usimamizi wa Huduma za Posta**

TCRA imeendelea kusimamia sekta ya Posta, ambapo kati ya July 2022 na Juni 2023, tumetekeleza yafuatayo :

- (a) Kutoa mafunzo kwa watoa huduma za usafirishaji wa vifurushi na vipeto kuhusu umuhimu wa matumizi ya anwani za makazi na postikodi, usalama na umakini ili kuzuia kusafirisha vitu hatarishi (prohibited items) mnyororo wa usafirishaji wa vifurushi na vipeto. Mafunzo haya yalitolewa katika kanda ya Mashariki, Kanda ya Kaskazini, Kanda ya Kati, Kanda ya Ziwa na Nyanda za Juu Kusini ;
- (b) Kuboresha Ubora wa huduma za Shirika la Posta kwa kushirikiana na Umoja wa Posta Duniani (UPU) kwa kuimarisha mfumo wa kusimamia Ubora wa Huduma za Posta (GMS One) katika ofisi za Posta Zanzibar, Mikoa ya Dar es salaam, Arusha, Kigoma, Mwanza Dodoma na Mbeya. Mfumo huu utatoa ufanisi udhibiti wa ubora wa huduma.
- (c) Kutoa Mada kwa wadau wa Sekta ya Posta (Kanda ya Mashariki) kuhusu mwelekeo Umoja wa Posta Duniani, ambao ni kuifungua UPU kwa wadau wengine zaidi wa Sekta ya Posta (*Opening up the UPU to wider sector postal players*). Kufunguliwa kwa UPU kunafuatia mageuzi ya sekta ya posta, ambayo yamesababishwa na kuwepo kwa kiwango kikubwa mwingiliano wa huduma za posta na huduma nyingine, ubinafsishaji wa mashirika ya posta na kuongezeka kwa shughuli za biashara ya mtandao duniani.

***Tunatoa rai kwa wananchi kutuma vifurushi na vipeto kwa watoa huduma ambao wamepewa leseni na TCRA ili kupunguza vitendo vya wizi pamoja na upotevu unaoweza kujitokeza na kujihakikishia usalama.***

## 2.8 Usimamizi wa usalama mtandaoni

TCRA imefanya usimamizi wa usalama mtandaoni kwa kufanya tathimini ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa lengo la kubaini madhaifu ya kiusalama na kushauri juu ya hatua za kurekebisha na kujilinda na matishio ya usalama mtandaoni.

Kufikia mwezi Juni 2023, TCRA ilifanya uchambuzi wa anwani za kompyuta zenye viashiria vya kushambuliwa na kutoa mashauri ya usalama mtandaoni (Security Advisories) kwa Taasisi za Umma na binafsi ambapo **mashauri 812** yalichambuliwa ukilinganishwa na mashauri **920** kwa kipindi kama hicho kwa mwaka wa fedha 2021/22 ili hatua stahiki ziweze kuchukulia kuimarisha usalama wa mifumo yao.

TCRA pia, inashirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao, Benki Kuu ya Tanzania na wadau wengine katika utekelezaji wa Muundombinu wa Saini za kieletroniki (National Public Key Infrastructure - NPKI) kwa lengo la kuboresha mazingira ya usalama wa Mawasiliano kati ya mtumiaji mmoja kwenda mwingine, kati ya taasisi moja kwenda nyingine hivyo kuwezesha kujilinda na matishio ya usalama mtandaoni.

## 2.9 Shughuli za TCRA kwa Kushirikiana na Taasisi za Kikanda na Kimataifa

Tanzania ni mwanachama wa mashirika mbalimbali ya kikanda na kimataifa. TCRA hushirikiana na taasisi za kimataifa na kikanda zinazosimamia mawasiliano na wadhibiti wa mawasiliano katika nchi nyingine na inatekeleza mikataba ya kimataifa katika sekta ya mawasiliano. Baadhi ya Taasisi na mashirika tunayoshirikiana nayo ni pamoja na

- (a) Mashirika chini ya Umoja wa Mataifa (United Nation Agencies) ambayo inajumuisha Shirika la Mawasiliano Duniani (International Telecommunication Union - ITU) na Umoja wa Posta Duniani (Universal Postal Union - UPU);
- ✓ Tanzania ilipata mafanikio makubwa ya kuleta ushindi wa kuwa Mjumbe wa Baraza la Mkutano Mkuu wa ITU katika Mkutano Mkuu wa ITU wa mwaka 2022 uliofanyika Bucharest, Romania mwezi Septemba 2022. ***Unachama wa Tanzania kwenye baraza hili unaifanya Nchi yetu kushiriki kwenye maamuzi muhimu yanayohusu shughuli za mawasiliano duniani.***

- (b) Mashirika chini ya Umoja wa Afrika (African Union Agencies) hii inajumuisha Umoja wa Posta Afrika (Pan African Postal Union - PAPU) na Shirika la Mawasiliano Afrika (African Telecommunication Union - ATU);
- ✓ TCRA kwa kushirikiana na PAPU zimesimamia na kuwezesha ujenzi wa Jengo la Makao Makuu ya PAPU ambalo lipo Mkoani Arusha kwa mafanikio. Ujenzi huu umekamilika na uzinduzi wake unatarajiwa kufanyika mwezi Agosti, 2023. ***Mikutano mikubwa ambayo hapo awali ilikuwa ikifanyika nchi nyingine, sasa itakuwa inafanyika Makao Makuu Arusha na kuwezesha ushiriki wetu kwa wingi zaidi katika kufanya maamuzi na pia kuchangia ukuaji wa sekta nyingine kama utalii.***
- (c) Taasisi za Jumuiya ya Madola inajumuisha Conference of Commonwealth Postal Administration (CCPA) na Commonwealth Telecommunications Organisation (CTO)
- (d) Taasisi za Kikanda za Mawasiliano: Shirikisho la Wadhibiti wa Mawasiliano Kusini mwa Africa (Communications Regulators' Association of Southern Africa - CRASA), Shirika la Mawasiliano la Africa Mashariki (East African Communications Organization – EACO), Shirikisho la Utangazaji la Kusini mwa Afrika (Southern African Broadcasting Association - SABA) Mtandao wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Afrika (African Communication Regulation Authorities Network – ACRAN).

## 2.10 Shughuli za Utafiti

Katika kipindi kuanzia Julai, 2022 hadi Juni 2023 TCRA ilifanikiwa kufanya tafiti mbalimbali katika maeneo yafuatayo:-

- (a) Utafiti wa gharama za mwingiliano wa huduma za mawasiliano ya simu Tanzania. Utafiti huu umepelekea kupatikana kwa gharama mpya za mwingiliano wa simu baina ya mitandao kuanzia mwaka 2022 hadi 2027. Gharama hizo, ikilinganishwa na mwaka 2022 ambapo zilikuwa **TZS 2.00, zimepungua hadi TZS 1.86 kwa mwaka 2023.** Mafanikio hayo yamechangia

kupungua kwa gharama za rejareja za upigaji wa simu baina ya mitandao, hivyo kuondoa ulazima wa wateja kuwa na laini za simu zaidi ya moja.

- (b) Utafiti wa wateja katika ulipaji wa ada za ving'amuzi - Utafiti mdogo katika kaya za Dar es Salaam. Utafiti huu ulibaini kuwa **83%** ya watazamaji wa TV mkoani Dar es Salaam hulipia vifurushi vya mwezi, 11% vifurushi vya wiki, na 6% vifurushi vya siku. Aidha, **57% ya kaya hizo hulipia vifurushi vya kati ya TZS 10,000.00 na 30,000.00**, **22%** vifurushi vya kati ya TZS **30,000.00 na 200,000.00**, na **21%** vifurushi vya kati ya TZS **1,000.00 na 10,000.00** kwa mwezi. Hata hivyo mwenendo wa ulipiaji wa vifurushi hivyo si wa mara kwa mara.


### 3.0 MWENENDO WA SEKTA

#### 3.1 Sekta ya Mawasiliano ya Simu na Intaneti

##### 3.1.1 Huduma za Simu

###### (a) Idadi ya Watumiaji wa Simu

Sekta ya Mawasiliano ya Simu nchini imeendelea kukua na hadi kufikia Juni, 2023 kulikuwa na **laini za simu Milioni 64.1** kutoka laini **Milioni 56.7** sawa na **ongezeko la 13%**. Idadi hii ya laini za simu inahusisha laini zinatotumiwa na watu na laini zinatumiwa kwa ajili ya mawasiliano kati ya mashine kwa mashine (M2M). Tunao watoa huduma sita (6) kwenye soko letu, yaani Airtel, Vodacom, Halotel, TTCL, Tigo na Smile. Mgawanyo wa asilimia za soko kwa kila mtoa huduma hadi kufikia Juni 2023 ni kama inavyoonyesha kwenye chati.



Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

Aidha, takwimu zinaonyesha kwamba mikoa mitano (5) Tanzania inayoongoza kwa kuwa na idadi kubwa ya laini za simu zinazotumika yaani (Active SIM-cards) hadi Juni 2023 ni: **Dar es Salaam (Laini Milioni 11,797,544), Mwanza (Laini 4,246,212), Arusha (3,858,283), Mbeya (3,687,622) na Dodoma (3,421,006).**

**(b) Gharama za Muunganisho wa simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine**

Gharama za Muunganisho wa simu kutoka mtandao mmoja kwenda mwingine zimekuwa zikipungua mwaka hadi mwaka. Mwaka **2015** gharama zilikuwa ni **TZS 30.58** na kwa sasa gharama zilizokokotolewa ni **TZS 1.86** kwa dakika. Hii inachangia kupunguza gharama za rejareja za upigaji wa simu na kuondoa ulazima wa wateja kuwa na simu zaidi ya moja.

**Mwenendo wa Gharama za mwingiliano baina ya mitandao hadi mwaka 2023**

Mwaka	2015	2016	2017	2018	2019	2020	2021	2022	2023
Uanishaji Na.3 wa gharama za mwingiliano (Determination No.3 of 2013 in TZS)	30.58	28.70	26.96						
Uanishaji Na.4 wa gharama za mwingiliano (Determination No.4 of 2017 in TZS)				15.60	10.40	5.20	2.60	2.00	
Uanishaji Na.6 wa gharama za mwingiliano (Determination No.6 of 2023 in TZS)									1.86


Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

**(c) Mwenendo wa gharama za rejareja kupiga simu bila ya kifurushi ndani na nje ya mtandao kuanzia 2015 – Juni. 2023 (zikijuisha kodi)**

Takwimu zinaonyesha kuwa wastani wa bei ya dakika ndani ya mtandao bila kifurushi (Tsh/dakika) zimeendelea kushuka kutoa **TZS 32 mwezi Julai 2022** hadi kufika **TZS 29, mwezi Juni 2023**.

Year	Wastani Bei ya Dakika Ndani ya Mtandao bila kifurushi (Tsh/dakika)	Wastani Bei ya Dakika Nje ya Mtandao bila kifurushi (Tsh/dakika)
2015	306	419
2016	300	405
2017	249	329
2018	248	321
2019	87	90
2020	72	73
2021	47	47
Julai.2022	32	32
Juni.2023	29	30

Mwenendo wa gharama za upigaji wa simu nje ya kifurushi zimeendelea kushuka kama zinavyoonyeshwa kwenye jedwali hapo chini. Kushuka kwa gharama za mwingiliano kumepolekea kuwa na tofauti ndogo sana ya gharama za kupiga simu ndani na nje ya mtandao.



Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

**(d) Wastani wa Bei za Vifurushi**

Wastani wa bei za kupiga simu kwa kutumia vifurushi zimekuwa zikibadilika mara kwa mara kutokana na gharama wanazotumia watoa huduma kufikisha huduma kwa mteja wa




mwisho kubadilika pia. Pamoja na mabadiliko hayo, gharama za kupiga simu ndani na nje ya mtandao zimekuwa na uelekeo wa aina moja na kukaribiana sana hivyo kumwezesha mteja kuwa na uhuru wa kupiga simu kwenda popote yaani ndani ya mtandao unaompa huduma na nje ya mtandao huo. Hali hii kwa kiasi kikubwa inaondoa ulazima wa kuwa na laini za simu za watoa huduma zaidi ya mmoja wote kwa wakati mmoja kwa lengo la kuepuka gharama.

### **Mwenendo wa gharama za rejareja kupiga simu kwa kutumia kifurushi ndani na nje ya mtandao kuanzia 2015 – Juni 2023 (zikijumuisha kodi)**

Vilevile, mwenendo wa gharama za rejareja kupiga simu kwa kutumia kifurushi ndani na nje ya mtandao kuanzia 2015 hadi sasa zimeendelea kushuka na kuwezesha watu wengi waweze kumudu gharama hizo. Julai, 2022 bei ya dakika ndani ya mtandao kwenye kifurushi (**Tsh/Dakika**) ilikuwa ni **7.7** na hadi kufikia Juni, 2023 bei imepungua kufika **5.19**.

<b>Mwaka</b>	<b>Bei ya Dakika Ndani ya Mtandao kwenye kifurushi (Tsh/Dakika)</b>	<b>Bei ya Dakika Nje ya Mtandao kwenye kifurushi (Tsh/Dakika)</b>
2015	10.46	17.99
2016	12.87	22.16
2017	10.04	18.3
2018	10.62	15.68
2019	9.46	18.51
2020	8.0	10.0
2021	8.4	8.8
Julai.2022	7.7	7.60
Juni.2023	5.19	6.3


Mwenendo wa gharama ndani na nje ya Mtandao ndani ya kifurushi zimeendelea kushuka na kukaribiana. Hali hii imechochea shughuli nyingi za kiuchumi kuweza kufanyika kupitia mawasiliano ya simu ukilinganisha na hapo awali. Hivyo kadiri siku zinavyokwenda watoa huduma wamekuwa wakishindana kwa ubora wa huduma wanayoitoa na sio gharama.



### (e) Gharama za SMS

Mwenendo wa bei za rejareja kwa SMS bila kifurushi na kwenye kifurushi kuanzia 2015 – Juni 2023 (zikihusisha kodi) nazo zimeendelea kushuka kwa sababu ya ushindani katika sekta. Katika mwezi Julai, 2022 bei ya SMS kwenye kifurushi (Tsh/Ujumbe) ilikuwa ni **3.1** na imeendelea kushuka ambapo mwezi Juni 2023 ilifika **1.41** kama inavyoonekana kwenye jedwali hapo chini;-

Mwaka	Wastani Bei ya SMS bila kifurushi (Tsh/Ujumbe)	Bei ya SMS kwenye kifurushi (Tsh/Ujumbe)
2015	82	2.96
2016	69	3.34
2017	51	2.4
2018	50	2.22
2019	35	4.46
2020	23	3.0
2021	20	3.1
Julai 2022	11	3.1
Juni 2023	11	1.41



Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

#### (f) Uwiano wa Mawasiliano ya simu kwa Idadi ya watu

Uwiano baina ya mitandao na matumizi unaonyesha kuwa maeneo mengi yamefikwa na huduma za Intaneti ila watumiaji ni wachache, sababu ikiendelea kuwa ni idadi ndogo ya watumiaji wenye simu janja, hivyo kupelekea kuwepo na umuhimu wa TCRA kufuatilia kwa kina gharama za simu janja. Pia muelekeo wa kufikia lengo la serikali la **80%** ya watumiaji wa huduma za Intaneti kufikia mwaka **2025** zinaendelea vema.

	Julai 2022	Juni 2023
<b>IDADI YA WATU</b>	61,741,120	63,150,477
Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 2G kwa idadi ya watu (2G Population Coverage)	98%	98%
Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 3G kwa idadi ya watu (3G Population Coverage)	72%	77%
Uwiano wa Mawasiliano ya simu ya 4G kwa idadi ya watu (4G Population Coverage)	55%	65%
Uwiano wa Mawasiliano ya simu kwa maeneo ya kiografia (Geographical Coverage)		
3G	55%	62%
4G	36%	50%
<b>Asilimia ya Simu Janja (Smartphone Penetration)</b>	25%	29%

Chanzo: Idadi ya watu ni kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS)

Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

#### (g) Ada za Mwingiliano wa Mawasiliano ya Simu za Kimataifa


Serikali imeridhia punguzo la ada za mwingiliano wa mawasiliano ya simu za Kimataifa kutoka **dola za Marekani senti 25/kwa dakika** hadi kiwango cha **dola za Marekani senti 10/kwa dakika**. Utaratibu huu umeanza kutumika mwezi Julai, 2023. **Hatua hii itachochea ukuaji wa uchumi ndani ya Jumuiya ya Afrika Mashariki.**

### 3.1.2 Huduma za Intaneti

Takwimu za sasa zinaonesha kuendelea kuongezeka kwa watumiaji wa Intaneti. Kwa kipindi cha mwaka mmoja uliopita **kumekuwepo na ongezeko la 17%** kutoka watumiaji **29,169,958**, mwezi Julai 2022 hadi kufikia **34,045,384** mwezi Juni 2023. Sababu kuu zinazochangia ongezeko la matumizi ya intaneti zimeendelea kuwa ni uwepo wa maudhui ya Kiswahili kwenye intaneti ikijumuisha kuongezeka kwa Program tumizi (applications) kwa lugha ya Kiswahili.

#### (a) Wastani wa Bei za Data (Tshs)

Mwenendo wa gharama za rejareja za data bila kifurushi na kwenye kifurushi kuanzia 2015 – Juni 2023 (ikijumuisha kodi) zimeendelea kupungua na kuongeza utumiaji wa huduma za Intaneti nchini kama inavyoonekana hapa chini:-



Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

#### (b) Gharama ya Data ukilinganisha na Nchi nyingine

- Kwa mujibu wa tafiti mbalimbali, hadi kufikia Juni 2023, Tanzania imeendelea kuwa nchi yenye kiwango kidogo sana cha bei ya data kwa GB 1 ukilinganisha na nchi nyingine za Afrika Mashariki (**Burundi, Kenya, Rwanda, Uganda, DRC, South Sudan na Tanzania**), ambapo gharama ya 1 GB ni Dola za Marekani 0.71 sawa na Shilingi za Kitanzania 1,666.
- Pia kwa kiwango hicho hicho Tanzania inashika nafasi ya **kwanza (1)** kwa bei ndogo ya data kwa GB 1 ukilinganisha na nchi zote zilizopo SADC (Malawi, Msumbiji, Zimbabwe, Afrika Kusini, Zambia, Botswana, Lethoto, Eswatini, Angola, Sychels, Comoro, DRC, Madagasca, Mauritius, Namibia, Tanzania ) na hii ni kwa

mujibu wa ripoti ya “Worldwide mobile data pricing 2022” inayopatikana kwenye tovuti ya <https://www.cable.co.uk/mobiles/worldwide-data-pricing/>.

- Tanzania pia inashika nafasi ya **saba (7)** kwa kuwa na bei ndogo ya data kwa Afrika hii ni kwa mujibu wa Takwimu zilizochapishwa katika tovuti ya Statista <https://www.statista.com/chart/29144/cost-of-mobile-data-in-africa/>. Katika **Bara la Afrika**, takwimu hizo zinaonyesha kuwa wastani wa **gharama ya 1 GB ni Dola za Marekani 3.51** hii ni sawa na **TZS 8,157**.

### 3.1.4 Huduma za Kifedha katika Mtandao wa simu

Tanzania inazidi kuendeleza mfumo jumuishi wa kifedha kutokana na kuongezeka kwa watumiaji wanaofanya miamala kupitia simu za mkononi. Takwimu za mawasiliano za mwezi Juni 2023 zinaonyesha kwamba huduma za pesa kupitia simu za mkononi zimeongezeka. Akaunti za pesa kwa simu za mkononi zimeongezeka na kufikia **47,275,660** Juni 2023 kutoka akaunti **38,008,482** mwezi Julai 2022 ikiwa ni ongezeko la **24%**.

Idadi ya miamala imeongezeka kutoka **349,952,830** Julai 2023 hadi miamala **420,675,884** Juni 2023. Aidha, akaunti za pesa kwa simu zimeongezeka kwa **24%** kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023; wakati miamala ikiongezeka kwa **20%**.

Mwezi	Mwaka	Idadi ya Watumiaji	Idadi ya Miamala
JULAI	2022	38,008,482	349,952,830
AGOSTI	2022	38,504,971	356,790,863
SEPTEMBER	2022	39,590,502	366,178,409
OCTOBER	2022	40,169,159	379,219,903
NOVEMBER	2022	40,353,939	378,344,304
DISEMBER	2022	40,953,496	410,741,935
JANUARI	2023	42,120,445	380,561,622
FEBRUARI	2023	43,172,914	370,853,274
MACHI	2023	44,353,568	421,094,958
APRILI	2023	44,940,441	407,480,068
MEI	2023	45,781,325	428,596,950
JUNI	2023	47,275,660	420,675,884

Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

### 3.2 Sekta ndogo ya Utangazaji

Takwimu za utangazaji zinaonyesha kwamba visimbuzi **3,342,626** vilikuwa hewani hadi Juni 2023 ikilinganishwa na visimbuzi **3,169,231** mwezi Julai, 2022. Kati ya hivyo, **1,700,205** ni vya dijitali kwa mfumo wa televisheni wa utangazaji wa mitambo ya ardhini (Digital Terrestrial Television - DTT) na **1,642,421** ni vya mfumo wa televisheni wa satelaiti.

**Dar es Salaam** inaongoza kwa kuwa na visimbuzi **(1,286,354)**, ikifuatiwa na Arusha **(275,449)**, **Mwanza (262,380)** na **Mbeya (208,924)**. Mikoa yenye **visimbuzi vichache** ni **Songwe (1,357)**.

Televisheni za waya (Cable TV) zimeenea kutoka watu **16,786** waliunganishwa 2018 hadi **19,671** Juni 2023. Huduma ya televisheni kwa waya (yaani Cable TV) imeenea mikoa ya Kanda ya Ziwa; ambapo **Mkoa wa Shinyanga unaongoza**; ukiwa na jumla ya waliunganishwa **2,803**, ikifuatiwa na **Mwanza, yenye 2,195** na ya tatu ni **Kagera** ikiwa na waliunganishiwa **1,770**. Mikoa yenye **wateja wachache** ni **Kilimanjaro (130)**, **Morogoro (120)** na **Pwani iliyounganisha wateja 30**.

Idadi ya Dikoda zinazotumika kwa kila Mtoa Huduma kufikia Juni, 2023 ikilinganishwa na Julai 2022 ni kama inavyoonekana kwenye jedwali hapa chini:-

MTOA HUDUMA	Julai 2022			Juni 2023		
	DTT	DTH	JUMLA	DTT	DTH	JUMLA
<b>Agape</b>	2,023	1,978	4,001	2,023	1,978	4,001
<b>Azam</b>	144,861	634,810	779,671	127,569	735,047	862,616
<b>Continetal</b>	40,443	26,289	66,732	39,137	27,615	66,752
<b>DiGiTek</b>	17,392	0	17,392	17,392	0	17,392
<b>DSTv</b>	0	203,532	203,532	0	227,066	227,066
<b>Star Times</b>	1,485,301	579,147	2,064,448	1,514,084	619,073	2,133,157
<b>Zuku</b>	0	33,455	33,455	0	31,642	31,642
<b>JUMLA</b>	<b>1,690,020</b>	<b>1,479,211</b>	<b>3,169,231</b>	<b>1,700,205</b>	<b>1,642,421</b>	<b>3,342,626</b>

Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

### 3.3 Sekta ndogo ya Posta

Katika kipindi cha hadi Juni tulituma nje ya nchi vipeto **230,347** na kupokea vipeto **138,699**. Huduma hii inaendelea kuchagiza ukuaji wa biashara mtandao (e-commerce).

#### Mwenendo wa Vifurushi na Vipeto vilivyotumwa na kupokelewa nchini

Mwaka	2017	2018	2019	2020	2021	2022	Juni 2023
Kutumwa nje ya nchi	10,121,388	5,098,728	2,873,312	1,116,069	564,528	239,239	230,347
Kupokelewa toka nje ya nchi	2,339,149	7,999,942	3,927,692	1,391,829	958,121	616,225	138,699

Chanzo: Takwimu za TCRA 2023

Aidha, siku za karibuni tumeshuhudia kupungua kwa watoa wa huduma za posta kutokana na changamoto zinazotokana na maendeleo ya TEHAMA ambayo yameleta njia mbadala ya mawasiliano. Pia kuwepo kwa watu binafsi wanaofanya biashara mtandaoni ambao wamekewa wakiagiza na kutuma vifurushi kutoka nje ya nchi.

### 4.0 CHANGAMOTO KATIKA SEKTA YA MAWASILIANO NA UTATUZI WAKE

Mtakumbuka kuwa mwaka jana tulikuwa na changamoto ya watoa huduma kutokuwa na bendi za kutosha za masafa ya kutoa huduma ambazo zina ubora zaidi na na masafa ya 5G. Pia kulikuwa na changamoto ya “*Right of Way*” ambapo, kama tulivyoeleza hapo awali, watoa huduma walitakiwa kulipa ada ya **Dola za Kimarekani 1000 kwa 1 Km** lakini sasa ada imepungua kufikia **Dola za Kimarekani 100 kwa 1 Km** kila mwaka.

TCRA katika kutekeleza majukumu yake inakabiliana na changamoto na utatuzi wake umeainishwa kama ifuatavyo:

Na	Aina ya Changamoto	Namna ya kukabiliana na changamoto
1.	Utoaji wa huduma za mawasiliano kwa wote kwenye	<ul style="list-style-type: none"> <li>TCRA imeendelea kushirikiana na wadau mbalimbali kama UCSAF, Watoa huduma za mawasiliano, TANESCO, Wakala wa Umeme Vijijini (REA), Wakala wa Barabara Vijijini</li> </ul>

Na	Aina ya Changamoto	Namna ya kukabiliana na changamoto
	maeneo ambayo hayajafikiwa bado.	(TARURA) pamoja na kuchangia katika Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ili kuhakikisha kuwa huduma za Mawasiliano zinafikishwa kwenye maeneo ambayo hayajafikiwa. Aidha, TCRA imeendelea kusimamia na kuhakikisha kuwa watoa huduma wanaendelea kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma wanazotoa kama inavyoelekezwa kwenye masharti ya leseni walizopewa ikiwa ni pamoja na kuchangia katika mfuko wa Mawasiliano kwa wote.
2.	Usalama wa Mtandaoni na Uhalifu wa Mtandaoni (Cyber security and Cybercrime).	<ul style="list-style-type: none"> <li>• TCRA kupitia kituo cha Kitaifa cha Usalama Mtandaoni (TZ-CERT) tunaendelea kusimamia usalama wa mtandao katika anga letu ikiwa ni pamoja na kutoa mafunzo kwa wadau.</li> <li>• TCRA imeendelea kushirikiana na Jeshi la Polisi katika kukabiliana na matukio ya uhalifu mtandaoni. Katika robo ya tatu ya mwaka 2022/2023 idadi ya majaribio ya uhalifu iliyorekodiwa ni jumla ya matukio <b>12,044</b>. Aidha, katika robo ya nne ya mwaka huo huo, majaribio ya uhalifu yalikuwa <b>23,084</b>.</li> <li>• Hii inaonesha kwamba kumekuwa na mwamko mkubwa wa utoaji taarifa za matukio ya uhalifu kupitia namba <b>15040</b> na <b>100 hivyo kudhibiti uhalifu</b>. Tunatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kuwasilisha taarifa za wahalifu mtandaoni kupitia namba hizo.</li> </ul>
3.	Kudhibiti Maudhui ya mtandaoni	<ul style="list-style-type: none"> <li>• TCRA inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali wakiwemo Watoa huduma za</li> </ul>



Na	Aina ya Changamoto	Namna ya kukabiliana na changamoto
		Utangazaji, Baraza la Sanaa Tanzania (BASATA), Bodi ya Filamu Tanzania (TFB) na wengineo katika kudhibiti maudhui mtandaoni
4.	Ubora wa Huduma za Mawasiliano	<ul style="list-style-type: none"> <li>TCRA imeendelea kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na watoa huduma zinakidhi viwango bora.</li> </ul>

## 5.0 MWELEKEO WA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZILIZOPANGWA KWA MWAKA 2023/24

Katika mwaka wa fedha 2023/24, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania inatarajia kutekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Tutaendelea kuwapa watumishi mafunzo endelevu ndani na nje ya nchi ili kukuza uwezo wao kwa utekelezaji wa kazi za udhibiti;
- (ii) Tutaendelea kuimarisha usimamizi wa Mfumo wa utoaji leseni na rasilimali za mawasiliano;
- (iii) Tutaendelea kutoa elimu kwa watumiaji na wadau wengine wa huduma za mawasiliano ili kuongeza uelewa juu ya haki na wajibu wao;
- (iv) Tutasimamia utekelezaji wa Muundombinu wa Kitaifa ya Mawasiliano ya Mtandao wa Umma (NPKI) ili kuhakikisha usalama wa miamala ya kieletroniki nchini;
- (v) Tutaendeleza kuboresha mifumo ya ndani ili kuongeza katika utendaji kazi ufanisi na kuendana na mabadiliko ya teknolojia yanayoendelea duniani;
- (vi) Tutaendelea kuimarisha upimaji na kusimamia ubora wa huduma za mawasiliano ili kutoa huduma za udhibiti kwa usahihi zaidi;
- (vii) Tutaendelea kusimamia usalama mtandaoni kupitia TZ-CERT kwa kufanya tathimini ya mifumo na miundombinu ya TEHAMA kwa lengo la kubaini madhaifu ya kiusalama na kushauri juu ya hatua za kurekebisha na kujilinda na matishio ya usalama mtandaoni;
- (viii) Tutahamasisha Uanzishaji wa Vikundi vya Kidijitali (Digital Clubs) Mashuleni na Vyuoni kwa ajili ya kujenga uwezo wa TEHAMA kwa Wanafunzi; na

(ix) Tutasimamia uimarishaji na upatikanaji wa mawasiliano ya Redio nchi nzima.

## 6.0 HITIMISHO

TCRA inaendelea kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sekta ya Mawasiliano kwa kushirikiana na wadau mbalimbali katika ngazi ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ili kuhakikisha Sekta ya Mawasiliano inatoa mchango katika maendeleo ya nchi na kuwa kichocheo cha ukuaji wa uchumi wa kidijiti na uchumi wa buluu.

**IMETOLEWA NA**

**MKURUGENZI MKUU**

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

**18 JULAI 2023**

